JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

## HALMASHAURI YA WILAYA YA MBINGA

**05/10/2023**

# KUKARIBISHA MAOMBI YA KUKODI MAGARI KWA KAZI MAALUMU

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya ya Mbinga inahitaji kukodi magari kwa ajili ya kazi maalumu itakayofanyika katika maeneo ya ndani ya Wilaya.

Mkurugenzi Mtendaji Wilaya ya Mbinga anakaribisha maombi kutoka kwa watu wenye magari yenye sifa zifuatazo;-

1. Gari liwe ni aina ya LANDCRUISER/ LANDROVER/ NOAH/ yenye uwezo wa kubeba ABIRIA WASIOPUNGUA 10.
2. Gari liwe na dereva mwenye leseni iliyo halali.
3. Gari liwe na Bima iliyo hai.
4. Gari liwe katika hali nzuri ya kukabiliana na milima na mabonde.

Wenye nia ya kukodisha magari yao kwa Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga wafike kwenye Ofisi za Mkurugenzi Mtendaji (W)-Mbinga kwa ajili ya kuchukua **fomu za maombi**.

Fomu za maombi kwa ajili ya kukodisha magari hayo zinapatikana ***bila malipo*** yoyote katika Ofisi ya Kitengo cha Ununuzi (PMU) iliyopo kwenye majengo ya Ofisi za Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga-Kiamili kuanzia saa 1.30 asubuhi hadi saa 9.30 alasiri jumatatu hadi ijumaa.

Maombi hayo yaandikwe na kutumwa kwa;

***Mkurugenzi Mtendaji (W),***
***Halmashauri ya Wilaya,***
***S.L.P 194,***
***MBINGA.***

Bahasha zenye maombi hayo zifungwe vizuri kwa lakiri na ziwasilishwe katika Ofisi ya Kitengo cha Manunuzi (PMU) iliyopo kwenye majengo ya Ofisi za Halmashauri ya

Wilaya ya Mbinga-Kiamili. Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 12-10-2023 Saa 5.00 Asubuhi na ufunguzi utafanyika siku na tarehe hiyo hiyo saa 5.00 Asubuhi katika ukumbi wa Kiamili Sekondari –Mbinga. Waombaji/wawakilishi mnakaribishwa kuhudhuria siku ya ufunguzi wa maombi hayo.

Maombi yote yatakayochelewa kulingana na muda uliotajwa hayatapokelewa, hayatafunguliwa, hayatasomwa siku ya ufunguzi na pia hayatazingatiwa katika kufanyiwa uchambuzi/tathmini kwa namna yoyote ile.

Andrew L. Mbunda.
Kaimu Mkurugenzi Mtendaji (W)
MBINGA

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA
MBINGA